FIDIA eNEWSLETTER

TOLEO LA TANO | JANUARI-MACHI 2025 | www.wcf.go.tz




# SERIKALI KUENDELEA KULINDA NA KUBORESHA USTAWI NA MASLAHI YA WAFANYAKAZI

## Yaliyomo

Miaka Kumi ya WCF: Kuendeleza uhusiano bora na wadau wote

Bodi mpya ya Wadhamini WCF yatakiwa kusimamia maslahi ya wanufaika na uhai wa Mfuko

WCF yatakiwa kuongeza kasi kusajili waajiri wote

# NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU



**DKT. JOHN MDUMA**
Mkurugenzi Mkuu wa WCF

## Mpendwa Msomaji

Kwa niaba ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), napenda kuwakaribisha katika toleo la tano la Jarida letu la Mtandaoni. Pamoja na mambo mengine mengi, habari kubwa katika Toleo hili ni kuhusu uzinduzi wa Shamra shamra za maadhimisho ya Miaka Kumi ya WCF ambao ulifanywa na Waziri wa Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Ridhiwani Kikwete mnamo Aprili 04, 2025 jijini Dodoma.

Katika kipindi hiki cha Miaka Kumi ya uhai wake, WCF imepiga hatua kubwa katika kutekeleza jukumu lake la kutoa fidia stahiki na kwa wakati kwa wafanyakazi. Mfuko huu ulianzishwa ili kulinda haki za wafanyakazi, na tumeona ongezeko kubwa la idadi ya wafanyakazi waliopata huduma zetu. Hii ni ishara ya mafanikio ya ushirikiano wa karibu na wadau wetu wote, ambao wamekuwa sehemu muhimu ya mafanikio haya.

Mwezi Juni, 2025 ni kipindi cha kipekee kwetu, kwani tunasherehekea kilele cha mafanikio yetu ya miaka kumi. Katika kipindi hiki kuelekea kilele cha maadhimisho haya WCF itatekeleza matukio maalum mbalimbali ambayo yatatoa fursa ya kuonesha na kusherehekea mafanikio yetu kwa wadau wetu.

Tunaposheherekea mafanikio ya miaka kumi, tunakumbuka na kuzitathmini changamoto zinazotukabili, lakini pia tunajivunia juhudi kubwa zinazochukuliwa ili kuhakikisha kila mfanyakazi atakayehitaji fidia anapata kwa wakati. Kwa upande wa mikakati yetu ya mbele, tumejipanga kuhakikisha kwamba Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi unaendelea kuwa na ushawishi mkubwa kwa kuongeza uwazi na ufanisi katika utoaji wa huduma, huku tukiimarisha ushirikiano wa karibu na Serikali na wadau wa sekta binafsi. Mikakati hii itasaidia kuongeza ufanisi na kupanua wigo wa huduma zetu kwa manufaa ya wafanyakazi wote wa Tanzania.

Tunawashukuru wadau wetu wote kwa kuendelea kutuunga mkono na kwa kushirikiana nasi katika safari hii ya mafanikio. Tuna imani kuwa kwa pamoja tutaendelea kufikia malengo yetu ya kuwalinda na kuwahudumia wafanyakazi wetu kwa ufanisi zaidi katika miaka mingi ijayo. Na hivyo tunapokaribia kilele cha maadhimisho yetu haya, tunapongeza juhudi za kila mmoja wetu zilizofanikisha mafanikio haya makubwa.

Karibuni na niwatakie usomaji mwema!.

Jarida hili limeandaliwa na
Kitengo cha Uhusiano kwa Umma WCF:
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,
S.L.P 329, 41104 Dodoma,
TANZANIA

# Fidia Mtandaoni



1. Usajili wa waajiri na hati ya usajili
2. Kuwasilisha taarifa ya mapato ya mwaka ya wafanyakazi
3. Kuwasilisha michango ya kila mwezi kupitia namba ya udhibiti na kupata stakabadhi
4. Kuwasilisha taarifa ya ajali, ugonjwa ama kifo kitokanacho na kazi
5. Kuhusisha taarifa za wafanyakazi na mwajiri
6. Kupata mrejesho madai ya fidia




**TIMU YA WAHARIRI**

MWENYEKITI
**Dkt. John Mduma**

MHARIRI
**Laura Kunenge**

MHARIRI MSAIDIZI
**Mcharo Mrutu**

WACHANGIAJI
**Meseka Kadala**
**Sophia Mtakasimba**
**Lilian Shembilu**

# SERIKALI KUENDELEA KULINDA NA KUBORESHA USTAWI NA MASLAHI YA WAFANYAKAZI-WAZIRI KIKWETE



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete akisaini kanuni zinazoanzisha fao jipya la Utengamao, tukio lililoenda sambamba na uzinduzi wa maadhimisho ya Miaka 10 ya WCF*

**Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete amesema Serikali itaendelea kutekeleza Kwa vitendo dhamira yake ya kuwalinda wafanyakazi ambao ni nguzo muhimu katika maendeleo ya Taifa.**

Mhe. Kikwete amesema hayo leo Jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Miaka 10 ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ambayo ina dhamana ya kulipa fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupatwa na ugonjwa unaosababishwa na kazi zao.

Amesema moja ya mikakati hiyo ni kuhakikisha kuwa WCF inaongeza wigo wa mafao ambapo hadi sasa inatoa jumla ya mafao saba ikiwemo Fao la Matibabu yasiyo na kikomo, Fao la Ulemavu wa Muda Mfupi, Fao la Ulemavu wa Kudumu, Fao la pensheni kwa wategemezi, Fao la Wasaidizi wa Mgonjwa, Fao la Utengamao na Fao la Msaada wa Mazishi.

"Serikali itaendelea kuzingatia matakwa ya mikataba ya kimataifa inayohusiana na maslahi na ustawi wa wafanyakazi wake, na katika kuthibitisha hilo ndio maana ikaanzisha Mfuko wa WCF", alisema Waziri Kikwete.

Mhe. Kikwete pia aliipongeza WCF kwa namna ilivyotoa kipaombele katika matumizi ya mifumo ya Tehama ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi.

"WCF imeboresha mifumo ya ushughulikiaji wa fidia kwa wafanyakazi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA ambapo hadi sasa zaidi ya asilimia 90 ya huduma zinazotolewa na zinapatikana mtandaoni, hali ambayo imeongeza ufanisi na tija katika utendajikazi wa Mfuko", aliongeza Mhe. Kikwete.



*Mhe. Kikwete katika uzinduzi wa maadhimisho ya Miaka 10 ya WCF.*

Katika hatua nyingine, Waziri Kikwete alisaini Kanuni zinazoanzisha fao jipya la Utengemao linalolenga kusaidia kumrudisha mfanyakazi aliyeumia kazini kuweza kuendelea na uzalishaji na utendaji kazi.



*Mhe. Kikwete na meza kuu*

Awali Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma alisema katika kipindi cha miaka 10 ya uhai wake, Mfuko huo umepata mafanikio lukuki ikiweo kupewa Cheti cha ithibati katika utoaji wa huduma bora kwa viwango vya Kimataifa (ISO Certification) mwezi Juni, 2024, hatua inayoongeza imani chanya kwa wadau wote wanaohusika kwenye mnyororo wa fidia kwa wafanyakazi nchini.



*Mhe. Kikwete na baadhi ya washiriki*

Maadhimisho hayo ya miaka kumi ya WCF yayotarajiwa kutamatika mwezi Juni mwaka huu yanachagizwa na Kauli mbiu isemayo "Miaka Kumi ya Fidia kwa Wafanyakazi: Kazi Iendelee".

# MIAKA KUMI YA WCF: KUENDELEZA UHUSIANO BORA NA WADAU WOTE




*Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi (Kulia) akipokea zawadi kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Bi. Laura Kunenge (wa pili kutoka kushoto)*

**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeweza kutekeleza majukumu yake kwa umahiri na mafanikio makubwa, katika kipindi cha miaka 10 mfululizo tangu kuasisiwa kwake.**

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kwa Umma wa WCF, Bi. Laura Kunenge, wakati alipokuwa akiwasilisha mada kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) uliofanyika Aprili 04, 2025 mjini Songea ambapo mgeni rasmi alikuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi.

Akiwasilisha mada kuhusu utekelezaji wa majukumu ya WCF katika kipindi cha miaka 10, Bi. Kunenge aliyaelezea mafanikio ya Mfuko huo katika kipindi hicho kuwa ni pamoja na kusajili waajiri kutoka sekta ya umma na binafsi, kulipa mafao kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata ugonjwa unaotokana na kazi zao pamoja na wategemezi wa mfanyakazi aliyefariki kutokana na kazi, kuwekeza kwenye maeneo yenye tija pamoja na kuimarisha mifumo ya kidijitali katika kusajili na kushughulikia madai ya wafanyakazi.

"WCF imekuwa na mafanikio katika maeneo mengi, ikiwemo kuongezeka kwa ulipaji wa mafao kwa wanufaika wa Mfuko, thamani ya Mfuko kuongezeka, lakini pia kutumia mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa kiasi kikubwa. Matumizi ya TEHAMA yameongeza ufanisi wa utoaji huduma kwakuwa hivi sasa mfanyakazi anayeumia au kuugua kutokana na kazi anaweza kuwasilisha taarifa kupitia mtandao, wakati wowote na kutoka mahali popote,' alisema Bi. Laura.

Aidha, Bi. Laura ameongeza kuwa WCF katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imepiga hatua kubwa na kusema wanaahidi kuendeleza ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo wana habari, wafanyakazi pamoja na Waajiri.

Mgeni rasmi, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, alikabidhi tuzo ya shukrani kwa WCF kwa kuwa miongoni mwa taasisi wezeshi katika mkutano huo uliomalizika Aprili 5, 2025 kwa kumchagua tena Bw. Deodatus Balile kuongoza TEF kwa kipindi kingine cha cha miaka minne.

ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

# BODI MPYA YA WADHAMINI WCF YATAKIWA KUSIMAMIA MASLAHI YA WANUFAIKA NA UHAI WA MFUKO



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete akizungumza wakati wa Uzinduzi wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo Bi. Renatha Rugarabamu na kulia ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Bi. Mary Maganga*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete amezindua Bodi mpya ya Wadhamini ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi – WCF, Machi 17, 2025 Jijini Dar es salaam.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mhe. Kikwete ameitaka Bodi hiyo kusimamia maslahi ya wanachama, uhai na uhimilivu wa Mfuko, na kuhakikisha kuwa uwekezaji unaofanywa na Mfuko unakuwa wenye manufaa. Mhe. Waziri aliitaka pia Bodi hiyo kufanya uchambuzi wa kina wa bajeti za Mfuko kabla ya kuzipitisha na kusimamia mali za Mfuko.

"WCF imekuwa na mafanikio makubwa katika maeneo yote ikiwemo kuongezeka kwa thamani ya Mfuko, kuongezeka kwa ulipaji wa mafao kwa wanufaika wa Mfuko na kutumia mifumo ya TEHAMA kwa kiasi kikubwa kwenye shughuli za Mfuko hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji huduma," alisema Mhe. Kikwete.

Akizungumza awali, Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma, amepongeza Bodi iliyomaliza muda wake kwa mafanikio makubwa ya Mfuko yaliyopatikana pamoja na kuuacha Mfuko ukiwa na uhimilivu wa kuendelea kuwalipa wanachama fidia wanapopata changamoto mahali pa kazi.




*Mhe. Kikwete katika picha ya pamoja na wajumbe wa Bodi mpya ya Wadhamini ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi*

# WCF NA JESHI LA POLISI WAWEKEANA MIKAKATI KUIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA UTENDAJI KAZI

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umetoa elimu kwa makamanda wa Jeshi la Polisi Nchini kuhusu umuhimu wao katika kuhakikisha wafanyakazi wanaopata madhila wakiwa barabarani wanapata haki ya fidia kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikaokazi hicho kilichofanyika jijini Dodoma hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma alitoa rai kwa maafisa hao wa jeshi la polisi kutoka mikoa na wilaya zote nchini kuusaidia Mfuko huo pamoja na wafanyakazi kwa kutoa taarifa za ajali za barabarani, na ajali za kikazi zenye viashiria vya jinai.

Dkt. Mduma alisema askari wa usalama barabarani ni wadau muhimu sana katika mchakato wa ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali zinazotokana na kazi, ambapo pamoja na mambo mengine kunahitajika taarifa ya polisi ili kukamilisha mchakato huo.

"Ili WCF iweze kulipa fidia za ajali za kikazi zinazotokea barabarani na ajali za kikazi zenye viashiria vya jinai, Sheria inataka kuwepo na taarifa za Polisi kama uthibitisho. Pamoja na mambo mengine, taarifa hizi za Polisi zinalifanya Jeshi la Polisi kuwa mdau wa kimkakati kwetu WCF," alisema Dkt. Mduma.

Kwa upande wake Kamishna wa Oparesheni na Mafunzo CP. Awadhi Juma Haji aliishukuru WCF kwa ushirikiano wake ambao imekuwa ikiutoa kwa jeshi hilo hususani katika kutoa elimu mbalimbali ambayo huwaongezea uelewa maafisa wake katika kukabiliana na vitendo vya kihalifu hasa vinavyohusiana na ajali za barabarani.

CP. Awadhi amesema kikao kazi hicho kinawawezesha maafisa wa polisi kukutana na kuweka mikakati ya kupunguza matukio ya ajali za barabarani. "Kikao hiki kinalisaidia . Jeshi la Polisi kuweka mikakati ya kudhibiti ajali za barabarani, na matukio haya yakipungua kutaiwezesha WCF kuokoa fedha nyingi ambazo zingetumika kuwahudumia wafanyakazi wanaopata ajali hizo," alisema CP. Awadhi.

Kikao kazi baina ya WCF na Jeshi la Polisi ni muendelezo wa vikao na mafunzo mengine ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano ya ushirikiano katika utendaji kazi (MoU) kati ya WCF na Jeshi la Polisi.

# Wanawake wa WCF wawashika mkono watoto wenye mahitaji maalum shule ya msingi Tandika




*Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kwa Umma wa WCF, Bi. Laura Kunenge akikabidhi mahitaji ya watoto wenye uhitaji maalumu kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Tandika, Mwl. Imamu Kassim Byoma*

Wafanyakazi wanawake wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) wametoa msaada wa mahitaji mbalimbali kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika Shule ya Msingi Tandika, Kitengo cha Watoto wenye Mahitaji Maalumu, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Kimataifa na miaka Kumi tangu kuanzishwa kwa Mfuko huo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kwa Umma wa WCF, Bi. Laura Kunenge, alisema kuwa Mfuko huo umejikita katika utamaduni wa kurejesha kwa jamii, hasa kwa makundi maalumu katika jamii yanayohitaji msaada.

"Tunatambua changamoto wanazopitia watoto hawa wenye mahitaji maalumu, na umuhimu wao kupata elimu, na kama taasisi, tumeona ni vyema kuwafikia kwa msaada huu ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuwahudumia, lakini pia kurejesha kwa jamii ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 10 tangu WCF ianzishwe," alisema Bi. Kunenge.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Msingi Tandika, Mwl. Imamu Kassim Byoma, aliishukuru WCF kwa msaada huo na kusisitiza kuwa ingawa Serikali inaendelea kugharamia mahitaji ya chakula kwa wanafunzi wa kitengo hicho, ni jukumu la jamii nzima na wadau mbalimbali kuiga mfano wa WCF kwa kushiriki katika kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalumu na siyo kuiachia Serikali pekee.

"Natoa wito kwa taasisi na watu binafsi kuiga mfano wa WCF kwa kusaidia makundi haya maalumu ili kuhakikisha wanapata mazingira bora ya kujifunza," alisema Bw. Kassim.
Msaada uliotolewa ni pamoja na viti vya kukalia wakati wa chakula, vifaa vya usafi, vyakula na mahitaji mengine muhimu kwa wanafunzi hao, jambo ambalo limepokewa kwa furaha kubwa na wanafunzi pamoja na walimu wa shule.

# WCF YATAKIWA KUONGEZA KASI KUSAJILI WAAJIRI WOTE

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Mhe. Ridhiwani Kikwete, amewataka watumishi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kuongeza nguvu katika kusajili waajiri na kuhakikisha kwamba wanawasilisha michango ya watumishi wao kwa wakati ili kuwezesha watumishi hao kupata haki yao kwa wakati endapo watapata ajali, kuumia, ugonjwa au kifo kutokana na kazi zao.

Waziri Kikwete aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, Machi 20, 2025 wakati wa kikaokazi kati yake na watumishi wa WCF kwa lengo la kujadili na kuelekezana namna bora ya kuboresha utendaji kazi.

"Natambua kuwa hadi sasa WCF imesajili asilimia 93.7 ya waajiri wote nchini, lakini hiyo haitoshi na ninaitaka menejimenti ihakikishe kwamba waajiri wote wanasajiliwa hadi kufikia asilimia 100 na wanawasilisha michango yao kwa wakati. Na katika hili ninawahimiza watumishi wote muwajibike kutekeleza jambo hili, kwa kuwa ndio msingi mkuu utakaosaidia kulipa fidia kwa wafanyakazi watakaopata ugonjwa, ajali au kufariki wakati wakitekeleza majukumu ya kazi.

Mhe. Kikwete pia aliagaiza Menejimenti ya WCF kuhakikisha inafanya uwekezaji katika maeneo yenye tija yatakayosaidia kuuongezea Mfuko uwezo wa kumudu kulipa fidia hususani katika maeneo ya hatifungani ambayo ni salama zaidi.

"Uwekezaji ni sehemu ya jukumu muhimu la WCF, na ili kuhakikisha eneo hili linakuwa na tija, basi mnapofikiria njia ya uwekezaji fikirieni maeneo yaliyo salama ili kuuwezesha Mfuko kumudu jukumu lake la msingi ambalo ni kulipa fidia kwa wafanyakazi wanaopata madhila kazini," alisisitiza

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma alisema kuwa Menejimenti imepokea maelekezo ya Mhe. Waziri na kwamba watumishi wataongeza kasi ya uwajibikaji ili kutekeleza maagizo hayo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Mhe. Ridhiwani Kikwete akizungumza na wafanyakazi wa WCF

"Tumepokea maelekezo ya Mhe. Waziri ambaye ametutaka kuongeza kasi katika usajili wa waajiri na ukusanyaji wa michango, jambo hili tumelipokea na tutalifanyia kazi," alisema

Akitoa salamu za shukrani mwakilishi wa wafanyakazi wa WCF, Bw. Musa Mwambujule alishukuru Mhe. Waziri kwa kutembelea na kuwasilkiliza wafanyakazi, jambo ambalo limeonesha namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inavyothamini wafanyakazi.



Baadhi ya wafanyakazi wakimsikiliza Mhe. Kikwete

# TUZO ZA MFANYAKAZI BORA WCF ZIWE CHACHU YA KUONGEZA KASI YA UTENDAJI KAZI



*Mfanyakazi bora wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Bw. Meseka Kadala kutoka Kitengo Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, akipokea cheti kutoka kwa Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini WCF Bw.Abdulaziz Shambe.*

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umetoa Tuzo za wafanyakazi bora katika kurugenzi na vitengo na Mfanyakazi Bora wa jumla, ikiwa ni sehemu ya kutambua na kuthamini mchango wa wafanyakazi wake.


Akizungumza wakati wa hafla ya utoaji tuzo hizo iliyofanyika Aprili 6, 2025 jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Rasilimaliwatu na Utawala wa WCF, Bw. Julius Lwenje alisisitiza umuhimu wa tuzo hizo katika kuhamasisha utendaji bora na kujitolea kazini. Alieleza kuwa tuzo hizo zinasaidia kujenga mazingira ya kazi yenye ushindani wa kimaendeleo na kuongeza motisha miongoni mwa wafanyakazi.

"Tuzo hizi ni ishara ya kuthamini kujitolea kwa mfanyakazi husika katika kutimiza majukumu yake, ushirikiano na jitihada za kuhakikisha malengo ya taasisi yanafikiwa.



*Wafanyakazi bora kutoka Idara mbalimbali katika picha ya pamoja*

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Bw. Meseka Kadala kutoka Kitengo cha Mahusiano kwa Umma alitwaa tuzo ya Mfanyakazi Kinara wa Mfuko wa ujumla ikiwa ni kutambua utendaji wake bora na mchango mkubwa katika kufanikisha malengo ya Mfuko.




**DIRA**

Mfano wa kuigwa katika utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi barani Afrika.

**DHIMA**

Kupunguza athari za kijamii na kiuchumi za majanga yatokanayo na kazi kwa wafanyakazi, familia zao na waajiri kwa kutoa fidia stahiki, kwa usawa, uendelevu na ufanisi.

# PICHA ZA MATUKIO MBALIMBALI












Jarida hili limeandaliwa na

Kitengo cha Uhusiano kwa Umma WCF:
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,
S.L.P 329, 41104 Dodoma,
TANZANIA

*MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI: KAZI IENDELEE*